



## Penye Wazee

- Amina:** Heheee dada huna habari?
- Rukia:** Sina habari.
- Amina:** Hujui Joho kaleta mke mpya?
- Rukia:** Katoka wapi?
- Amina:** Katoka huko kijijini.
- Rukia:** Kijiji gani?
- Amina:** Kijiji kimoja kinaitwa Handeni.
- Rukia:** Mamaa? Ni kijijiiii!! Na anavyoringa basi!
- Heheeee, haloo!
- Amina:** Kila akipita ana kanga mpya, akirudi ana kanga mpya.
- Rukia:** Heee! Jamani si kavaa kanga mpya kwa ajili ya kujisitiri mwili wake?
- Amina:** Hahaa! Mimi sitaki kukuhadithia mengi akipita utajionea mwenyewe akipita tuu utamwona yaani akipita kavaa kanga mpya, akirudi kavaa kanga mpya.
- Rukia:** Atapita saa ngapi? Mimi nataka nimwone.
- Amina:** Utamwona tuu maana kila siku anapita hapa hapa.
- Rukia:** Yaani nakaa mtaa wa mbali nakosa mengi, yaani leo nitakaa hapahapa mpaka jioni ili nimwone.
- Amina:** Shoga umemwona?
- Rukia:** Heheee! Huyo anapita angalia kanga ilivyoandikwa.
- Amina:** Imeandikwaje?
- Rukia:** "Tutabanana hapa hapa!"
- Wote** (wakicheka) hahaaaaaaa

**Rukia:** Si bora angenioa mimi?

**Amina:** Joho kapotea kabisa!

**Amina:** Juzi juzi katoka kijijini alivaa kanga imeandikwa jogoo la shamba haliwiki mjini hapa ni mjini babu.

**Rukia:** Heheeeee! Katukuta hapa mjini bwana.

**Amina:** Na akirudi sokoni anapita na kanga nyingine?

**Rukia:** Sijui anaachaga dukani halafu anakuja na nyingine?

**Amina:** Shoga yangu mimi hizi mboga sinunui tena kwa yule mama.

**Rukia:** Ameniuzia mboga zimekomaa tunatupa tuu mboga.

**Amina:** Yule mama unampenda mimi nilikuambia uende kwa mama Tabu.

**Rukia:** Si unajua ni mteja wangu wa kila siku shogaa. Sasa tutachanganya na nini ili mboga itoshe mpaka jioni?

**Amina:** Shoga nikuambie kitu ? Tuchambue mboga, tupike, halafu unisindikize kwa shangazi.

**Rukia:** Kwa shangazi kuna nini tena?

**Amina:** Nina shida naye tu.

**Rukia:** Shida gani?

**Amina:** Kwani mpaka ujue yote?

**Rukia:** Kwani ni mgonjwa?

**Amina:** Wala haumwi.

**Rukia:** Naenda kumsalimia tu.

**Amina:** Ni salamu tu.

**Rukia:** Hujamwona siku nyingi?

**Amina:** Ni kweli sijamuona siku nyingi. Shoga jirani yako vipi?

**Rukia:** Atapita tu maana huu ndiyo muda wake.

**Amina:** Hahaaaaa! Siyo kitu cha kuuliza hicho.

**Rukia:** Joho naye katuacha sisi wa mjini anaenda kuoa wa kijijini.

**Amina:** Tunatakiwa tukaoge na maji ya baharini!

**Rukia:** Ndugu yangu tutachubuka!

**Amina:** Heheee! leo kavaa kanga imeandikwa “Njama zenu nimezisikia nasubiri vicheko vyenu!”

**Wote:** Heheeee

**Rukia:** Cheko lako hilo. Hebu chambua mboga siye tukapike.

**Mpita njia:** Haya, naomba niwaulize.

**Amina:** Hehee una jipya?

**Mpita njia:** Naomba kuuliza, kwanini kila nikipita hapa wenzangu mnanicheka?

**Amina:** Dada tumekucheka saa ngapi?

**Mpita njia:** Kila nikipita ni mimi tu mnanisema. Samahani naomba niwaulize?

**Amina:** Utuulize nini?

**Mpita njia:** Kwa nini kila nikipita mnanicheka mimi?

**Amina:** Umejuaje kama tunakucheka wewe?

**Mpita njia:** Maana kila nikipita mnanicheka mimi.

**Amina:** Wewe dada una hila, kwanza ukipita hapa hata husalimii, na kila siku unapita na vikanga vipya.

**Mpita njia:** Kila siku nikipita nawasalimia lakini hamwiitikii.

**Amina:** Wewe dada una hila lo!!! Wewe ni wa shamba tuu hapa mjini huna Lako!

**Rukia:** Unaenda, unarudi na kila siku unatupita tu hata husalimii, una hila sana wewe dada.

*Baada ya muda kidogo ...*

**Bibi:** Kuna nini tena wajukuu zangu?

**Wote:** Bibi shikamoo?

**Bibi:** Marhaba wajukuu zangu, mbona kuna kelele kuna nini tena?

**Wote:** Afadhali bibi umekuja.

**Mpita njia:** Bibi kila nikipita hawa watu wananisema mimi, na kunicheka mimi.

**Bibi:** Mnatakiwa mpatane, mwelewane na pia msaidiane.

**Wote:** Tusamehe sana dada yangu.

**Mpita njia:** Mimi nimewasamehe.

**Wote:** Ama kweli penye wazee hapaharibiki neno.

**Amina:** Karibu sana dada tutakuwa tunakusuka kila siku.

**Mpita njia:** Asante sana.

**Amina:** Karibu hata ukae.

**Rukia:** Karibu sana tunajua kusuka mitindo ya aina zote kama zigizaga, twende kilioni n.k.

**Mpita njia:** Kumbe mnajua hata kusuka?

**Wote:** Ndiyo karibu sana.

**Mpita njia:** Karibu sana.